

UNAWEZA KUCHANGIA KWA NJIA GANI?

PIGA KURA KWA BUSARA!

Uchaguzi wa Kenya unaokuja ndani ya 2022. Wajue wagombea na piga kura kwa hekima kwa maswala unayoyajali. Mwaka huu, tunaandaa misururu ya vyipindi nya Facebook live na viongozi wa Mombasa na wagombea viti mbali mbali. Shiriki na ulize maswali yako!



JISHIRIKISHE!

Ni rahisi kwa wanasiada kutupuuza wakati tunapokaa nyumbani na kulalamika. Ni ngumu sana tunapojoitokeza kwa nguvu na kuwasilisha suluhu zinazofichua kujihusisha kwao na rushwa, Kutokuwa na Uwezo wa kufanya kazi na urafiki. Counti inapoandaa vikao nya kijamii, jitokeze, na uongee!



AMBIA RAFIKI!

Hakuna mtu atatakaye Okoa Mombasa pekee yake. Nguvu kwa idadi ni muhimu. Wakati unapiga kura, muhimize rafiki yako afanye vivyo hivyo. Unapohudhuria vikao nya kijamii, mlele rafiki yako pia. Hamasisha, eneza ujumbe na usaidie kulijenga vugu vugu la Okoa Mombasa!



#OKOA**MOMBASA**

WANACHAMA

- Ajenda Kenya
- Dock Workers Kenya
- Fast Action Summit
- Haki Yetu Organisation
- InformAction
- Human Rights Watch
- Kenya Long Distance Trucks Union
- Kenya Transporters Association
 - Mombasa residents
 - Muslims for Human Rights
 - Taireni Association
- Stella Maris International



www.okoamombasa.org



@Okoamombasa



Okoamombasa

OKOA MOMBASA NI NINI?



MJI WA MOMBASA UNAKUFA. UNAFAA KWUA UNANAWIRI.

Mombasa ni mji uliobarikiwa na wingi wa rasilimali za asili. Unafaa uwe Tajiri sana. Ila unanyongwa: Reli ya Kisasa ya SGR imeuwa bandari yetu kwa kuhamisha kazi zetu bara. Watu wanaishi na umaskini wakati wasomi wanapora rasilimali zetu.

TUNAPIGANIA MJI WETU TENA.

Okoa Mombasa ni muungano wa wananchi husika wanaopigania siku za usoni za mji wa Mombasa. Lengo kuu ni kuhakikisha ushirika wa ndani kwa rasilimali za ndani. Wakaazi wa mji wa Mombasa lazima wajihushe katika maamuzi yanayodhuru rasilimali na maisha yao.



TUNAPIGANIA NINI?



Ushiriki wa umma



Uhuru kutoka kwa umaskini



Fursa sawa




Mshikamano

Mombasa imeathirika na tatizo sugu la jamii kutojihusisha na kufanya maamuzi yanayoathiri county yetu. Hatuonekani kwa viongozi wetu. Ndio maana vugu vugu la Okoa Mombasa linahimiza uraia tendaji kazi kukuza haki ya jamii kujihusisha kikamilifu kwa maswala ya kijamii, kisiasa na Maisha ya kiuchumi. Kupitia kujihusisha kikamilifu na kwa umoja, tunaweza kujinasua kutoka kwa dhuluma na umaskini na kuifanya upya Pwani.




MAELEKEZO YA USAFIRISHAJI SHEHENA KWA RELI YA KISASA (SGR)

Changizo kuu la kudorora kwa Mombasa limesababishwa na maelekezo ya serekali yanayosurutisha usafirishaji wa shehena kutoka bandarini kupitia kwa reli ya kisasa. Maelekezo haya yamechangia kufungwa kwa mamia ya biashara Mombasa, maelfu ya ajira kupotezwa na kudorora kwa uchumi wa Mombasa. Tunapigania kubadilisha miongozo hii iliowekwa kinyume cha sheria.



ZABUNI YA RELI YA KISASA

Reli ya kisasa (SGR) ni mradi ghali zaidi katika historia ya Kenya na ulifadhibiliwa kwa njia kubwa na Uchina kupitia mikopo. Lakini huduma zake hazizai mapato yanayotosheleza kulipia madeni hayo. Licha ya haya, zabuni ya mkopo wa reli ya kisasa (SGR) hajawahi kuwasilishwa kwa uma. Serekali inajribu kuficha nini? Je serekali ya Uchina itachukua bandari ya Mombasa? Tumeenda mahakamani kushurutisa serekali iweke wazi zabuni hiyo.



HIFADHI YA WATERFRONT

Majina ya mahali ni sehemu muhimu sana kwa tamaduni na urithi wa jamii. Lakini hifadhi ya Mombasa iliokarabatiwa hivi karibuni imepewa jina la mke wa aliyekuwa rais wa kwanza wa Kenya "Mama Ngina". Jina hili halina uhusiano na Mji wa Mombasa. Tunapigania kwamba hifadhi hiyo ibadilishwe jina litakaloashiria historia na urathi wa mji wa Mombasa. Na tunataka jina jipya lichaguliwe kwa kushirkisa jamii.



TERMINAL YA SHEHENA 2 (CT2)

Terminal ya shehena 2 ni ya kisasa zaidi katika bandari ya Mombasa - rasilimali kuu kwa Kenya. Lakini serekali inajaribu kubinafsisha CT2 kwa njia isio ya kawaida kutajirisha watu binafsi. Hii itachangia kuotezwa kwa nafasi za kazi zaidi ya 4,500. Tunapigania kuzuia ubinafsishaji wa bandari ya Mombasamahakamani na tunataka wakaazi wa Mombasa wajighusise na maamuzi yatakayoathiri Bandari ya Mombasa.